



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAFIA



Tarehe: 28/09/2022

TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia anayo furaha kutangaza nafasi 3 za ajira ya kudumu kwa Watanzania wote wenye sifa stahiki **Dereva Daraja II**. Nafasi za ajira hii inarudiwa kutangazwa na inatokana na Kibali cha ajira kutoka kwa **Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora** kwa barua **Kumb. Na. FA.97/228/01/9** ya tarehe **13 Mei, 2022**.

1. DEREVA DARAJA LA II (NAFASI 3)

2.1 SIFA ZA MWOMBAJI:

- Awe na elimu ya kidato cha nne
- Awe na leseni ya daraja E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha ufundi stadi (VETA) au chuo chochote kinachotambuliwa na serikali
- Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi Daraja la II (Drive Test II) watapewa kipaumbele

MSHAHARA:

Mshahara unaanza na ngazi ya **TGS B**

2.3 KAZI ZA KUFANYA:

- I. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini usalama wa gari
- II. Kufanya matengenezo madogo madodo ya gari
- III. Kujaza na kutunza taarifa za safari katika daftari la safari (Log Book)
- IV. Kufanya usafi wa gari
- V. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- VI. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- VII. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake

2. MAELEZO YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE

- a) Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa
- b) Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika na majina matatu ya wadhamini wa kuaminika
- c) Mwombaji awe Raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45
- d) Mwombaji lazima aandike anuani na namba za simu pamoja na majina na anuani za wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika
- e) Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya taaluma, nakala ya cheti cha kidato cha nne au sita kilicho halali, nakala ya vyeti vya kuhitimu mafunzo
- f) Mwombaji aambatanishe picha mbili ndogo (passport size) za hivi karibuni zenye rangi kwa muono wa nyuma (Background)
- g) Testimonials, Provisional results, statement of results, hati za matokeo ya kidato cha nne au sita **HAZITAPOKELEWA.**
- h) Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na Mamlaka husika (NACTE, NECTA, TCU, n.k)
- i) Waombaji waliostaafishwa/kufukuzwa kazi katika Utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba.
- j) Uwasilishaji wa sifa na vyeti vya kughushi na ikabainika wahusika watachukuliwa hatua stahiki za kisheria
- k) Maombi yaandikwe kwa mkono na mwombaji kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza
- l) Waombaji wote kwenye barua zao za maombi waandike namba za simu za uhakika kwa ajili ya mawasiliano.


MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI TAREHE 12 OKTOBA, 2022 SAA 9.30 ALASIRI.

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Mafia,
13 Barabara ya Boma,
S.L.P 85,
61782 MAFIA.



Tangazo hili linapatikana kwenye mbao za matangazo za Halmashauri, Tovuti ya Halmashauri www.mafiadc.go.tz na Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira www.ajira.go.tz



**KASSIM S. NDUMBO,
MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA MAFIA**

